**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM**

**CHUO CHA USTAWI WA JAMII**

# TAARIFA KWA UMMA

**PROGRAMU YA LABOUR RELATIONS AND PUBLIC MANAGEMENT**

Kijitonyama, Dar es Salaam; 22/05/2024

Chuo cha Ustawi wa Jamii kilianzishwa kwa Sheria ya Bunge Na 26 ya mwaka 1973 (kama ilivyorekebishwa kwa sheria Na 03 ya mwaka 2002). Lengo kuu la kuanzishwa kwake ilikuwa ni kutoa mafunzo, kufanya tafiti na kutoa ushauri wa kitaalamu katika fani za Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Jamii na nyingine zinazoshabihiana na hizo.

Kama ilivyo kwenye Vyuo vya Elimu ya Juu, Programu za Chuo cha Ustawi wa Jamii zina ithibati kutoka Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi (NACTVET).

Hivi karibuni kumekuwepo na upotoshaji kupitia mitandao ya kijamii kuwa Programu ya ***Labour Relations and Public Management*** inayotolewa na Chuo Cha Ustawi wa Jamii haitambuliki katika Soko la Ajira.

Tunapenda kuutaarifu Umma kwamba programu ya ***Labour Relations and Public Management*** inatambulika katika Soko la Ajira na wahitimu wetu wameajiriwa katika Taasisi mbalimbali za Umma na za Binafsi na wengine wamejiajiri wenyewe. Mfano, katika sekta ya Umma, wahitimu wa programu hii wamekuwa wakiajiriwa kama Maafisa Rasilimali Watu, Maafisa Utawala, na Maafisa Kazi kwenye Wizara na Halmashauri mbalimbali hapa nchini.

Hivyo, tunapenda kuujulisha Umma kwamba taarifa hizo hazina ukweli na zina lengo la kupotosha Umma.

Imetolewa na Kitengo cha Mawasiliano
**Chuo cha Ustawi wa Jamii**